TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI
SHULE YA SEKONDARI VWAWA
S. L.P 224 MBOZI SONGWE

TANZANIA, SIMU 0755 535 637/ 0753 707 894/0734 285 188

KUMB NO. VSS/B/11 Tarehe…….

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE HII

Mpendwa mwanafunzi_____

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **TANO CBG, HGL, HKL, EGM** na **HGK** mwaka **2022/2023** katika shule ya sekondari Vwawa. Unatakiwa kuripoti shuleni ndani ya siku **kumi na nne (14)** kuanzia tarehe ya kufungua shule. **Tafadhali ripoti mapema.**

Pamoja na barua hii naambatanisha orodha ya **vifaa ambavyo lazima uwe navyo, sheria za shule, kanuni za shule ambazo unatakiwa uzifuate kwa muda wote utakokuwa mwanafunzi wa shule hii, nakala ya cheti cha kuzaliwa, fomu ya uthibitisho wa afya yako, fomu ya taarifa binafsi ambazo unatakiwa kuzikamilisha kabla haujafika shuleni, pamoja na fomu ya kukubali nafasi ya shule**. Kumbuka kipimo cha maendeleo yako ni taaluma, kazi za nje pamoja na nidhamu yako ndani na nje ya shule kwa muda wote utakao kuwa shuleni hapa.

Mzazi/Mlezi na mwanafunzi, mnatakiwa kusoma /kujaza maelekezo hayo kwa umakini ili kuepuka usumbufu siku za baadaye . Aidha kwa wanaotoka mbali mahitaji mengi yanapatikana katika soko la Vwawa.

Aidha, Shule ipo Mkoa wa Songwe, Wilaya ya Mbozi, Nusu kilomita kutoka Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya.

Karibu Vwawa sekondari.

_____

FAINES C. MAGWAZA
MKUU WA SHULE

ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE

a) Ada ya shule kwa mwaka shilingi 70,000/= mwanafunzi utalipa shilingi elfu 35,000/= kwa muhula kupitia akaunti namba **61201000008** NMB Jina la akaunti ni VWAWA SECONDARY SCHOOL. Tafadhali andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye pay in slip. Pindi afikapo shuleni aiwasilishe kwa Mhasibu wa shule.

b) Michango mingine inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

i. 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho
iii. 20,000/= kwa ajili ya taaluma (kwa mwaka) iv. 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine (kwa mwaka)
v. 2,000/= nembo ya shule
vi. 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza
vii. 5,000/= tahadhali (haitarejeshwa)
viii. 10,000/=Mchango wa Mahafali (sh5,000/= kwa kila mwaka).
ix. 20,000/= Kwa ajili ya mitihani endelezi.

NB: Ada na michango yote ya shule ilipwe kupitia akaunti tajwa hapo juu.

Jumla ya Ada na michango mingine ni Tsh.188, 000/=

c) MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI:-

i. Ream ya karatasi 2(kwa mwaka)
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa)
iii. Scientific calculator iv. Godoro la futi 3(3 X 6)
v. Mashuka pair 2 rangi ya blue bahari, blanketi 1, foronya 1 na chandarua 1.
vi. Passport size nne (4).
vii. Soksi nyeupe nzito zisizo na maua jozi mbili, kiatu cheusi cha ngozi na cha kamba kisicho na kisigino kirefu na raba nyeupe ya kamba. viii. Mavazi mengine ni nguo za ndani za kutosha ,taulo, blankenti mbili (2), mashuka mawili (2) rangi ya (blue bahari), bed cover lisilotariziwa maua yoyote, mto, foronya nyeupe, sanduku imara lenye kufuli na chandarua rangi nyeupe.
ix. Kijiko cha kulia chakula, sahani na kikombe,
x. Ndoo mbili za lita 10 za kuogea na kutunzia maji

AJE NA;

- Spring file (1).
- Mkebe (mathematical set), calculator kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi.
- Madaftari makubwa (Counter books angalau three (3) quire) za kutosha, peni, penseli na rula.
- Mwamvuli.
- Laboratory Coat 1(white color).(CBG) Begi la kubebea daftari.
- Toilet papers za kutosha.
- Sare ya shule sketi mbili za malinda moja ya rangi ya machungwa (orange) na nyingine rangi ya zabibu (blue violet) zinazofika kwenye kisigino (ndefu).
- Mashati meupe mawili(2) ya mikono mirefu na sweta rangi ya damu ya mzee(Maruni).
- Viatu vyeusi pea moja visivyo na kisigino kirefu na Raba nyeupe pea moja (isiyo na mchanganyiko wa rangi yoyote) ya kamba isiyo na kisigino kirefu) kwa ajili ya kuvaa darasani.
- Tai moja (1) ya Orange.
- Rangi ya Ijabu kwa waislamu ni nyeupe (White) na rangi ya waridi (Pink) kwa muda usio wa darasani.
- Nguo za kazi au gauni mbili rangi ya blue mkapa.
- Track suit rangi nyeusi isiyobana chini na raba kwa ajili ya michezo
- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika visipungue viwili (orodha imeambatishwa)
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

❖ **MUHIMU: MWANAFUNZI AJE NA NAKALA YA HATI YA MATOKEO (RESULT SLIP) YA KIDATO CHA NNE.**

VIFAA VYA USAFI VINAVYOHITAJIKA SHULENI:

Kutokana na uhaba wa vitendea kazi hapa shuleni mwanao aje na vifaa vifuatavyo:

i. CBG Walete drier 1, Hard broom 1 na Toilet brush 1.
ii. EGM Walete hard broom 1, panga moja gumu na imara na soft broom
iii. HGK walete leki, soft broom1, Hard broom 1
iv. HKL na HGL Walete mopa na ndoo yake ya kudekia 1

ANGALIZO KWA MZAZI/MLEZI

1. Mtoto akishapokelewa shuleni, Mzazi/Mlezi au ndugu yeyote harusiwi kuja kumwona labda uitwe na uongozi wa shule au ikitokea sababu isiyozuilika.

2. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu na kifaa chochote cha simu, vyakula vya aina yoyote na mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mtu wa nje ya shule yafanyike tu kupitia uongozi wa Shule.
3. Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevaa sare ya shule

TAARIFA BINAFSI:

1. Jina lako kamili lilivyotumika kidato cha nne……
   Dini/dhehebu……..
2. Jina kamili la Baba Mzazi/Mlezi……
   Kazi yake…….
   Anwani kamaili ya Baba Mzazi/Mlezi……
   Namba za ya simu ya mkononi……
   Namba yake ya simu ya mezani……..
   Mahali anakoishi Baba Mzazi/Mlez: Mkoa……..... Wilaya……
   Tarafa…….....Kijiji/Mtaa…….

3. Jina kamili la Mama Mzazi/Mlezi……
   Kazi yake…….
   Anwani kamaili ya Mama Mzazi/Mlezi……
   Namba za ya simu ya mkononi……
   Namba yake ya simu ya mezani……..
   Mahali anakoishi Mama Mzazi/Mlez: Mkoa……..... Wilaya……
   Tarafa…….....Kijiji/Mtaa…….
4. Hapa Songwe nina/sina ndugu
   Endapo una ndugu jaza jedwali lifuatalo na bandika picha zao.

NB: Kila mwanafunzi analazimika kuja na nakala ya cheti cha kuzaliwa

FOMU YA KUKUBALI

1. **Sehemu ya Mwanafunzi**

Mimi…….ninakubali nafasi niliyopewa kidato cha tano mwaka……. Katika shule ya Sekondari Vwawa na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kuwa nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni……

2. **Sehemu ya Mzazi/Mlezi**

Mimi …….....ninakubali mtoto wangu……. Kuchukua nafasi kuingia shule ya sekondari Vwawa na nitafika shuleni bila kuchelewa.Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake wa shule na Taifa. Na nitafuatilia maendeleo yake kitaaluma, tabia na mwenendo wa mtoto wangu nikishirikiana na walimu.

Anuani yangu ya kudumu ni…….

……

Namba ya simu……..

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandashi.

Sahihi…….. tarehe……..

NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

VWAWA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 224,
MBOZI.
DATE……

To:
THE MEDICAL OFFICER,
…….
…….
……
Please examine…….
As to her fitness for pursuing further education at this school.

1. Haemoglobin……..
2. P.V.Blooding……..
3. (A) Blooding……. (B) Hearing……..
4. Blood Pressure……
5. Urine for Sugar and Pregnancy tests…….
6. Stool for routine examination…….
7. Asthma…… 8. Skin diseases…….
9. Leprosy……
10. Pulmonary tuberculosis……..
11. Employs……..
12. Deformity……..
13. Mental problem……..
14. Comments……

.....
…….
……
……..

DESIGNATION

SHERIA ZA SHULE

Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa asijihusishe na makosa yafuatayo hapo chini vinginevyo anaweza kufukuzwa/kufutwa shule.

1. Wizi.
2. Kutohudhuria masomo bila taarifa.
3. Uasherati na ushoga.
4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya.
5. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake/walimu/walezi.
6. Uvutaji wa bangi.
7. Makosa ya jinai.
8. Kupigana na kupiga.
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
10. Kudharau Bendera ya Taifa.
11. Kuolewa au kujihusisha na mapenzi.
12. Kupata mimba, kufanya jaribio la kujiua.
13. Kutoa mimba.
14. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
15. Kukataa adhabu kwa makusudi.
16. Kuingia kwenye virabu vya pombe,nyumba za kulala wageni na katika kumbi za sitarehe.
17. Kulala nje ya shule bila ruhusa(Utoro).
18. Kuwasha mshumaa bwenini/kukutwa na kiberiti.
19. Kushiriki matendo ya uahalifu, Siasa.
20. Kumiliki kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika Mazingira ya shule.

KANUNI ZA SHULE

A. HESHIMA

Kila mwanafunzi anatakiwa uzingatia yafuatayo:-

1. Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Kutotumia lugha mbaya ,wakati wowote kati yao wenyewe ,kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Kuwa na **kucha fupi zisizopakwa rangi na nywele fupi pia ziwekwe katika hali ya usafi kila wakati,** kuvaa mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbia aliko mkuu anayekuita.
8. Kuheshimu ukumbi wa mikutano,mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya Umma.
9. Kusimama katika msitari wakati wa kupokea huduma.
10. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo.
11. Kunyosha mkono juu na usimame unapouliza au kujibu maswali.
12. Kukaa kimya wakati wote unapokuwa darasani, usitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
13. Kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zilizopo katika Jamii.
14. Ni marufuku mwanafunzi kuja shuleni na **redio na hita**

B. MAHUDHURIO

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.
2. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kuhudhuria katika kazi za mikono.
4. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa,mikutano ya nyumba na madarasa.

C. MAANDALIO YA JIONI

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na Jumapili saa 1:30 hadi saa 4:00 usiku.ispokuwa siku ya Jumamosi ambapo wanafunzi wanaruhusiwa kuangalia tv katika ukumbi wa shule.

   Mwanafunzi haruhusiwi kukaa au kulala bwenini muda huo ukipatikana adhabu itatolewa dhidi yake.

2. Walimu wa zamu watasimamia maandalio ya jioni kikamilifu.

D. SHERIA ZA SARE YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa 1. Masomo darasani.

2. Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
3. Baraza la shule.
4. Kwenda hospitalini.
5. Kwenye maandamano rasmi.
6. Wanaposafiri kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo.
7. Kazi za mikono **(vazi la kazi).**
8. Michezo.

MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:-

1. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mku wa shule.
2. Ni kosa kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu:
   (a) Chumba cha waalimu (Staffroom).
   (b) Ofisi za shule.
   (c) Maabara.
   (d) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

E. UGONJWA

1. Endapo kutakuwa na tatizo lolote la kiafya mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu, na kwa matroni wa shule. Mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa yoyote bwenini. Dawa zote zitunzwe kwa matroni.
2. Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika sehemu maalumu kwa kibali cha matron na endapo atazidiwa atapelekwa hospitali.
3. Mwanafunzi mwenye matatizo lazima aufahamishe uongozi wa shule au Matron wa shule, mara afikapo shuleni.
4. Shule haitoi CHAKULA MAALUMU **(Special** diet**)** kwa mwanafunzi mgonjwa.

F. ANGALIZO KWA MWANAFUNZI

1. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule.
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kukutwa na kitu chochote kinachohusisha mapenzi mfano barua, daftari lenye nyimbo za mapenzi **n.k.**
3. Ni kosa mwanafunzi kupita eneo lisilo na barabara maalumu au kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni kwa ajili ya kutunza Mazingira ya shule.

MWANAFUNZI ANASHAURIWA KUJA NA VITABU VISIVYOPUNGUA VIWILI (2) VYA MASOMO ANAYOSOMA, VITABU VYA ZIADA (REFERENCES) KAMA IFUATAVYO:-

1. **CHEMISTRY(1$2)**
    a) Chemistry Advanced Chemisrty Review by William W. Davis (Mzumbe book shop project, 2004)
    b) 2. Physical chemistry by Delungu, et (Mzumbe book shop project, 1998)
    c) 3. Advanced Level Inorganic Chemistry part I and II.(Tanzania instate of education ,1995)
    d) 4. Organic Chemistry volume I. The Fundamental Princinples by I.L. Finar (Longman Ltd 1990
2. **ENGLISH**
    a) Advanced learner's English language for Tanzania secondary school by Abraham Mulungu
    b) Advanced level English by Nicholous Asheri
    c) Advanced level English language 1by shadrack ndambo and James Kinunda
3. **HISTORY**
    a) Lesson notes for advanced certificate of secondary education (history paper one and history paper two) by Bakari Madaya
    b) Essential in advanced level history paper 1by salehe Yasin
    c) Essential in advanced level history paper 2 by Salehe Yasin
    d) Learning advanced African history book one by Idrisa R Msuya
    e) Learning advanced World history book two by Idrisa R Msuya
    f) Fundamental principles of history one by Mangoti B
    g) Fundamental principles of history two by Mangoti B
    h) Modern world history by Ben Walsh

4. **ECONOMICS**
    a) Essentials for economics 1 by Odhiambo Ambrose
    b) Essentials for economics 2 by Odhiambo Ambrose
    c) Economics for advanced level paper 1 by Ambilikile C.M
    d) Economics for advanced level paper 2 by Ambilikile C.M
5. **MATHEMATICS**
    a) Advanced mathematics for advanced level Book 1$2
    b) Conceptual advanced mathematics for secondary schools form v $ vi
    c) Advanced Mathematics Vol. I and ministry of education and vocational training
    d) Advanced Mathematics by shayo
    e) Advanced Mathematics by Tranter and Laube
    f) Pure Mathematics vol. I and II by Back House
    g) Further Pure Mathematics by Bostock and Chandler Rourke
6. **GEOGRAPHY**
    a) J.W.NJIKU , The essential of practical Geography A level
    b) **D.T.**MSABILA, An intergrated focal region on Human and Economic Geography-A level
    c) **D.**T MSABILA(2019) Comprehensive Approach to Physical Geography A level
7. **KISWAHILI**
    a) Kiswahili shule za sekondari fasihi kidato cha tano na sita (TET)
    b) Kivuli kinaishi (saida Mohamed)
    c) Mfadhili (Hussein tuwa)
    d) Vuta nikuvute (shafi adam shafi)
    e) Kunga za fasili na lugha (msokile 1992)
    f) Sarufi ya Kiswahili sekondari sekondari na vyuo (mdee) Dup-Dsm
    g) Historia ya kiswahili Afrika mashariki (Shiragrin na mnyampala)
    h) Tafsiri na ukalimani (mwansoko)
8. BIOLOGY
    a) New Understanding Biology By Suzan Toole
    b) Advanced biology principles and application by C.J. Clegg and D.G. Mackean
    c) Advanced biology by Michael Kent
    d) Dissecting Kit.(compulsory)